



Research Article



Check for updates

Section: Literature, Linguistics & Criticism



Published in Nairobi, Kenya
by Royallite Global.

Volume 6, Issue 1, 2022

**Article Information**

Submitted: 5th October 2021

Accepted: 31st December 2021

Published: 2nd January 2022

Additional information is
available at the end of the
article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

ISSN: 2520-4009 (Print)

ISSN: 2523-0948 (Online)

To read the paper online,
please scan this QR code

**How to Cite:**

Juma, J., Chimera, R., & Mutiti, Y. (2022). Uchanganuzi wa mafumbo katika nyimbo za taarab za Siti Binti Saad. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences*, 6(1). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/njhs/article/view/711>



Uchanganuzi wa mafumbo katika nyimbo za taarab za Siti Binti Saad

Juma Nyongesa Job¹, Rocha Chimera² na Yakobo Mutiti³

Chuo Kikuu cha Pwani, Kenya

Barua Pepe: jayjuma52@yahoo.com

<https://orcid.org/0000-0001-9105-8686>

Ikisisri

Makala hii imeangaza muhutasari wa nyimbo na maana ya mafumbo yanayojitokeza katika nyimbo za Taarab za Siti Binti Saad. Maana ya mafumbo katika nyimbo hizi yamehusishwa na utamaduni wa Waswahili katika Upwa wa Afrika Mashariki. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Semiotiki na ile ya Mtindo. Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na wa maktabani. Kuna data za msingi ambazo zilikusanywa nyanjani na za upili ambazo zilipatikana kwenye vitabu maktabani. Nyimbo ziliteuliwa kimakusudi kwa vile ni nyimbo zilizojulikana sana. Makala haya yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ili kubainisha aina mbalimbali za mafumbo. Katika ufafanuzi wa mafumbo katika nyimbo hizi maudhui ainati yalijitokeza. Kazi hii inalenga kuwafaidi wanafunzi wa fasihi katika uelewaji wa jinsi ya kuchanganua mafumbo. Vilevile, nyimbo za Siti zitaweza kuhifadhiwa kupitia kwa utafiti huu. Makala hii itakuwa kumbukumbu ya nyimbo za Siti.

Utangulizi

Nyimbo za Taarab ni mojawapo ya vitambulisho vya mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki. Yeyote aingiaye katika Pwani hii, hukaribishwa kwa nyimbo hizi za Taarab. Nyimbo za Taarab zina historia ndefu hasa tangu maajilio ya Waarabu katika upwa wa Afrika mashariki. Nyimbo hizi zimesheheni na kutawala mioyo ya watu wengi katika sehemu nyingi za kanda la Afrika Mashariki. Pwani, visiwani na maeneo ya mwambao wa Afrika Mashariki ndiyo asili na fasili ya muziki wa Taarab. Wapenzi wa muziki huu huutumia kwa kujifurahisha na kupata mafunzo ya kijamii. Muziki huu wa Taarab ulianza hapo miaka 100 iliyopita Unguja, na hivyo Unguja ikatambuliwa kama makao makuu ya Taarab. Khamis (2016), anasema kuwa nyimbo za Taarab ziliendelezwa na kina Siti Binti Saad, Bi Kidude, Juma Bhalo na kina Sheikh Ilyas Mchapurula bila kuwasahau mamia ya wanawake na wanaume wa Unguja na wa Mrima waliochangia maendeleo ya tasnia hii adimu. Siti alizuru sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki hata ulimwengu mzima akitumbuiza watu kwa nyimbo za Taarab.

Nyimbo nyingi za Taarab zinasheheni matumizi ya mafumbo kama mbinu ya lugha (Kea, 2006). Matumizi ya mafumbo katika nyimbo za Taarab hudhihirisha athari ya mazingira katika utunzi na uimbaji wa nyimbo hizi. Jamii ya Waswahili ilikuwa na matumizi ya mafumbo kama mtindo wa lugha yao. Kwa mujibu wa Harries (1962), katika historia ya Waswahili kulikuwa na mashindano ya kufumbua mafumbo. Yule ambaye alikuwa na uwezo wa kufumba shairi alikuwa anajulikana kama shaha. Hili linaashiria kuwa mashairi ya kimapokeo yalikuwa na matumizi ya mafumbo. Mashairi ya Taarab ya kiasili hayaangalii tu mlingano wa vina na mizani, bali pia maudhui na mantiki ya kile kilichomo- tena kikiwa kwenye mafumbo yanayoweza kusikika vyema. Ni muziki ambao hutungwa kwa ufundi au usanii mkubwa wa lugha. Ufundi huu hupelekea watu wachache kuelewa na kupata ufahamu wa nyimbo za Taarab zikiwemo za Siti.

Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani ili kuweza kukusanya nyimbo za msanii Siti Binti Saad. Utafiti wa nyanjani ulifanyiwa katika maeneo ya Unguja na Mombasa. Watafiti walikuwa ni watu wenye ufasaha wa nyimbo na mashairi ya Taarab. Aidha, waliteuliwa kwa njia ya makusudi. Sampuli kusudio kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), ni mbinu inayomruhusu mtafiti kutumia vijenzi maalum vya idadi lengwa na ambavyo huwa na habari ambayo mtafiti anaihitaji akiongozwa na malengo ya utafiti husika. Hali kadhalika, mtafiti alitumia uteuzi-tajwa kwa ambao hutajwa na wenzao, yaani mtu anayemhoji anamtaja mwingine ambaye anaweza kukupatia data unazohitaji. Baadhi ya watafiti walihojiwa ili kuweza kupata maana ya nyimbo mbalimbali. Watafiti hawa pia walieleza visa ambavyo viliambatana na nyimbo za Siti. Kuna nyimbo za Siti ambazo zilihusiana moja kwa moja na mikasa iliyokuwa ikitokea huko Unguja. Kwa hivyo, mbinu ya mahojiano ilitumika katika ukusanyaji wa data. Utafiti ulifanywa katika maeneo ya Unguja na Mombasa. Nyimbo za Siti zilisikizwa kwa makini kisha kunukuliwa daftarini. Hatua ya pili ilikuwa ni kutambua nyimbo ambazo zinaakisi malengo ya makala haya ya kubainisha mafumbo na maana inayopatikana katika mafumbo haya. Kwa hivyo, nyimbo ambazo zilikuwa na mafumbo ziliweza kuchanganuliwa na mafumbo kubainishwa.

Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu ulitumia nadharia mbili, nadharia ya Mtindo na nadharia ya Semiotiki. Nadharia ya Mtindo iliasisiwa na Buffon (1930) ilhali nadharia ya Semiotiki iliasisiwa na Uswizi Ferdinand de Saussure (1857-1913), pamoja na mwanafalsafa wa Kimarekani Charles S. Peirce (1839-1914). Nadharia hii ya

Mtindo iliendelezwa na Leech (1969) na Coombes (1969). Coombes alidai kwamba ili kuchanganua mitindo katika kazi fulani ni lazima vipengele vinavyofanya kazi hiyo ivutie vizingatiwe. Coombes anazungumzia vigezo kama vile matumizi ya taswira, wazo la kishairi, hisia zinazoibuliwa, uteuzi wa maneno, urari wa maneno na urari wa vina. Mawazo makuu ya de Saussure (1966) aliyeleza kuhusu mtazamo wa kisemiotiki yalizingatia zaidi ishara za kiisimu zinazohusu maana ya msingi au maana halisi bila kuangalia maana batini ya ishara husika. Mifumo hii ni sehemu ya utamaduni japo imekabidhiwa mipaka maalum na maumbile ya lugha. Nadharia hii inatufundisha namna ya kufahamu matumizi ya lugha ya ishara. Aidha, inaeleza kile ishara hizi zinarejelea katika kazi ya fasihi.

Mafumbo katika nyimbo za Taarab za Siti

Sehemu hii inadokeza maana ya mafumbo katika nyimbo za Siti. Nyimbo mbalimbali zimeelezwa. Maudhui mbalimbali yamejitokeza katika harakati za kueleza mafumbo katika nyimbo hizi. Maudhui ya mapenzi ndiyo yamejitokeza sana ingawaje kuna maudhui mengine kama ya siasa na uongozi.

Wimbo Kijiti

Wimbo huu unaeleza kisa cha kweli kilichotokea kisiwani Unguja. Msimbo wa kimatukio ulitufaa kwa kufumbua mafumbo aliyotumia Siti katika wimbo huu. Tuliweza kusimuliwa kisa kilichopelekea wimbo huu kuimbwa. Jambo hili lilitupelekea kungamua wimbo mzima. Siti hakuwa akiimba tu kuwafurahisha watu; baadhi ya nyimbo zake zilikuwa na mikasa halisi. Mwanamke mmoja alifika kutoka Dar-es-Salaam na kwenda Zanzibar kutembelea shoga yake. Mwanamke huyu aliyejulikana kama 'mgeni' kwa maana ya kuwa na ugeni katika sehemu ya Unguja. Mama huyu mgeni alikuwa na bwana aliyekuwa na jamaa huko Unguja. Bwana huyu alimshawishi mke wake (mgeni) kwenda kuwatembelea jamii yake Unguja. Mgeni alifungiwa safari na akafika Ng'ambo si mji Mzee wa Unguja. Hapo alikuwa mwenyeji wa Bi. Subeti aliyeishi karibu na sehemu Siti alikuwa ameolewa chuo cha pili, nyumba zimeelekezana milango. Mgeni alikuwa mwanamke mrembo anayependeza na alipotandikiwa mkeka akatokea mwanamume mmoja akapendezwa naye. Yule bwana akajaribu kumshawishi mwanamke yule mgeni lakini akashindwa. Akaenda kwake ingawa kwa kinyongo. Alipofika kwake aliwaeleza vijana wenzake kile kilichotokea wakamueleza aende kwa Bi. Kijiti akitaka kumpata huyo mwanamke mgeni. Kijiti alikuwa mjanja kwa haya maswala ya ulaghai. Kazi yake Kijiti ilikuwa ya kuwapatia mabwana wanawake ili wajitosheleze kwa mapenzi. Huko Unguja wafanyajikazi hii ya kuwapa mabwana waume walijulikana kama kuwadi.

Mwanamume huyu alipofika kwa Kijiti, alimuomba Bi. Kijiti kumfanyia mpango ili aweze kumpata mwanamke huyo mgeni kwa urahisi. Kijiti alimkubalia tajiri bila tatizo lolote. Kijiti alimsihi mgeni huyo kuandamana na bwana huyo kwenye magoma ya starehe za kijinga za mwanamume huyo huko Mkokotoni Unguja. Walienda sehemu inayoitwa Sharif Musa, iliyoko kaskazini kilomita takribani kumi na sita kutoka mjini. Walipofika huko yule mwanamume alimlaghai yule mwanamke mgeni akanywe pombe nyingi. Kwa kufanya hivi yule mgeni mwanamke alilewa zaidi. Mwanamke huyu mgeni hakuwa makini na hila za mwanamume huyu tajiri. Tajiri katili aliwezakumpata kwa urahisi kisha alimbaka mwanamke huyu pamoja na wanaume wengine. Mwishowe mgeni huyu aliishia kuaga dunia. Tajiri alimrusha barabarani huyu mwanamke mgeni. Siti wakitoka Mkokotoni katika shughuli zao za taarab na mwenzake wakiwa katika taksi wakauona mwili wa huyu mwanamke mgeni. Dereva wa tekisi akaamua kuutazama ule mwili kwa makini wakathibitisha kuwa ni mwili wa mgeni wa mwenzao. Dereva akaona amueleze mwenyeji wa yule mwanamke mgeni kuhusu kifo chake. Dereva wa tekisi alijulikana kama Sumaili.

Baada ya tokeo hilo, tajiri huyo aliishia kutoa hongo ili kukomesha kesi hiyo. Hakimu wa kesi hiyo hakuhukumu kwa haki na ukweli. Alitupilia mbali kesi hii baada yakupokea mlungula. Mashahidi wa kesi hii ndiyo waliofungwa badala yake. Habari hii imetokana na mahojiano kati ya mtafitiwa na mzee Amer Bin Amer Bin Suod wa Unguja Bwejuu tarehe 15/8/2020.

Anwani ya wimbo huu *Kijiti* inajitokeza kama fumbo. Kijiti ni kipande cha mti aghalabu huwa ni chembamba. Mara nyingi kijiti kinaweza kutumika kama bakora inayotumika kwa kuadhibia watu hasa watoto wakorofi. Muhusika mkuu katika wimbo huu anatumika katika kumutesa yule mwanamke mgeni. Alipomlaghai kuwa waende na mwanamume tajiri kwenye starehe za pombe kisha mgeni yule anaishia kubakwa. Kule kubakwa ni adhabu ingawaje mgeni yule hakustahili adhabu hiyo kwani hakuwa na makosa. Mkosa aliyestahili adhabu kali ni haini mwanamume tajiri. Mfano katika ubeti:

Tazameni tazameni, aliyofanya kijiti
*Kumchukuwa mgeni, **kumchezesha foliti***
***Kendanae maguguni**, kumrejesho maiti*
Kendanae maguguni, kumrejesho maiti

Neno maguguni limejitokeza kama fumbo katika wimbo huu. Maguguni ni majani ya mimea tofauti tofauti midogo midogo iliyoota sehemu na kushikana. Ambapo wadudu hatari huweza kujificha. Siti aliashiria mahali ambapo mambo mabaya yanaweza tokea. Katika jamii hii ya Wanzanzibar, unywaji pombe na vitendo vya haramu mara nyingi hutendeka maguguni. Maguguni ni sehemu ambayo mambo ya haramu hutendeka mara kwa mara. Msitari wa 'kucheza foliti' una maana fiche. Kulingana na TUKI (2004), foliti ni mchezo wa watoto wa kujificha na kufukuzana au kibe. Kwa hivyo, Kijiti alimchezea mgeni mchezo wa kumlaghai au kumhangaisha. Alimdanganya waende kwa anasa kumbe alikuwa na njama ya kumwangamiza mwanamke huyo. Alijifanya mzuri kumbe alijificha kwa uzuri. Alikuwa na lengo lingine tofauti kando na unywaji wa pombe. Tazama mfano katika ubeti huu:

Tuliondoka nyumbani, hatuaga ruhusa
***Na tende yetu kapuni**, tumechukua kabisa*
Magoma yako Chukwani, mauti

Tende ni aina ya pombe ambayo ilitumiwa sana ingawa ilikuwa imaharamishwa wakati huo. Hutengenezwa kwa mchanganyiko wa matunda yaliooza, matunda hayo huchanganywa na sukari iliochemshwa ili kutenga mvuke. Mvuke huo ndio ulevi, huitwa tende au gogo. Katika wimbo huu kijiti alipewa kinua mgongo cha kumzubaisha huyu mgeni. Mgeni analalamika kuwa kijiti alimua kwa sababu ya tende moja. 'Tende' lina maana ya pombe au aina ya tembo. Pombe hii ndiyo iliyotumika kumsubaisha yule mwanamke mgeni. Siti anaendeleza hali hii ya kulaghaiwa kwa mgeni kwa kusema kuwa mgeni na Kijiti waliondoka wakiwa tayari wameahidiwa pombe na starehe. Anasema kauli hii kwa fumbo, na 'tende yetu kapuni, tumechukua kabisa'. Mfano katika ubeti:

Tuliondoka nyumbani, hatuaga ruhusa
***Na tende yetu kapuni**, tumechukua kabisa*
Magoma yako Chukwani, mauti

Walielekea kwa sehemu ya starehe baada ya kushawishiwa kwa tende. Starehe anazihusisha na neno magoma. Kwa kawaida magoma huchezwa mahali kwenye sherehe fulani au starehe. Baada ya kitendo hiki Kijiti na bwenyenye yle walihepa mkono wa sheria kwa kutoa mlungula. Mfano katika ubeti ufuatao:

*Mambo haya ni ajabu kila tukiyatizama
Kijiti kauwa mtu tumboni mna mwana
Kijiti kuvuka mto mashahidi wamezama*

Kirai 'kuvuka mto' kina maana fiche. Kijiti na tajiri yule aliyembaka mwanamke mgeni walitoa pesa nyingi kwa hakimu wa ile kesi. Hali hii inamuezesha tajiri na Kijiti kuhepa mkono wa sheria hali ambayo inajitokeza kama kuvuka mto. Mashahidi katika kesi hii ndiyo wanaonaswa na kufungwa. Katika hali ya kawaida watu huvuka mto kwa kuogelea au kutumia dau. Katika wimbo huu tajiri na Kijiti wanatumia pesa na kumhonga hakimu. Mashahidi ni watu ambao ni muhimu sana katika kesi au katika uamuzi wa jambo lolote. Katika kesi hii ya Kijiti na tajiri, jaji anawahukumu mashahidi badala ya kuwahukumu waliokosa, yaani tajiri na Kijiti. Mambo kuwaharibikia mashahidi ndiyo maana ya 'kuzama'. Neno zama kwa mjibu wa (TUKI) 2004 ni kuingia ndani ya maji au kwenda chini. Vilevile lina maana ya kutoweka machoni usionekane. Kesi kutupiliwa mbali ndiyo maana inayojitokeza katika muktadha wa wimbo huu. Siti anamuonya Kijiti kuwa asikanyage Dar es Salaam. Huko atakumbana na hali ngumu kwa unyama wake aliomtendea mwanamke mgeni. Mfano katika ubeti:

*Kijiti nakuusia Dar es Salaam usiende
Utamkuta kitabu kakuvulia kikwembe
Watu wanakuapiza Mola akupe matende*

Sentensi 'utamkuta kibabu kakuvulia kikwembe' ina maana ya ndani. Kikwembe ni kishuka kifupi kilichokuwa kikivaliwa na wavuvi wa zamani wakiwa baharini. Vazi kuvuliwa iliashiria hali ya makabiliano kati ya Kijiti na bwana huyo. Katika wimbo huu ina maanisha kuwa Kijiti angepata adabu iwepo angefika jijini kwa vile angeondolewa ukatili wake na babu. Ishara ya kumvilia kikwembe ni kuwa tayari kwa vita. Lakini kutokana na neno hili kikwembe kudhoofika kimaana sasa vijana na watu wazima wanaoishi maeneo ya mjini hutumia kumaanisha mtu ambaye hatulii kwenye mahusiano yake ya mapenzi yaani mtu asiye kuwa na mpenzi mmoja. Katika wimbo huu maana ya kitambo itatumika kumaanisha makali ambayo watu wako nayo kwa Kijiti huko mjini. Hawana mzaha au imani naye tena, ni hasidi wao. Kibabu anawakilisha watu ambao wanamachungu na Kijiti.

Wimbo 'Muhogo wa Jang'ombe'

Wimbo huu wa Siti una mambo mengi ambayo yamefichwa katika lugha ya mafumbo. Wimbo huu unazungumzia kuhusu unywaji wa pombe ambao uliwapoteza wanaume. Wanaume wengi waliishia kupotelea kwa pombe kisha kukosa heshima hata kwa wake wao. Siti mwenyewe anasema kuwa hajashiriki unywaji wa pombe. Mlevi anapolemewa kwa pombe huanguka chini na huwa amelegea sana. Jang'ombe ilikuwa sehemu ya mashambani (porini) maarufu kwa kileo. Walevi wengi walikuwa wakijificha kwa vile ulevi ulikuwa umepigwa marufuku na serikali ya Sultan. Tabia mbovu za walevi mbovu za kuwachezea wanawake ziliweza kajulikana kila sehemu.

Siti anasema kuwa walevi wameshiriki ulevi kwa kutumia rupia (aina ya pesa wakati huo) nane na hata gilasini pombe imekamilika haipo. Walevi wanagombana kuthibitisha ikiwa ni kweli pombe imekamilika. Kwa hivyo, chupa rupia nane ni kiwakilishi cha fedha zilizotumika katika kugharamia tembo iliyonywewa na walevi. Kisha kupewa chupa kutazama na ishara ya majibizano ya walevi baada ya kubugia kileo. "Nipe nami nione, nipe nami nione", kauli ya walevi. Mfano katika ubeti:

*Muhogo wa Jang'ombe, Sijauramba mwiko
Usitukane wakunga, na uzazi ungaliko
Chupa rupia nane, tumekunywa watu wanne
Gilasini imekwisha, nipe chupa nitazame' :*

Anwani ya wimbo huu 'Muhogo wa Jang'ombe' ina maana ya ndani. Jangombe ni sehemu maalum kule Unguja. Ni sehemu iliyokuwa ya mashambani na ilitambuliwa kwa kilimo, lakini kwa sasa ni mji mkubwa sana. Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne Mpya (2001) muhogo ni mmea fulani ambao katika jamii ya Waswahili huandaliwa kama chakula. TUKI (2004) inaeleza muhogo kama mmea wenye sina lenye vidutu na moyo mwororo ambao unaza mihogo ambayo huliwa. Jamii ya Waswahili inathamini sana chakula hiki cha muhogo. Ingawaje hutegemea na sehemu; kuna aina mbalimbali ya mihogo. Aina hii pia huwa tofauti kwa utamu wake. Katika wimbo huu Siti anausawiri muhogo kama pombe itokayo Jango'ombe. Vile jamii ya Waswahili wanavyothamini muhogo ndivyo walevi walivyothamini pombe ya Jang'ombe. Mwimbaji anasema kuwa mlevi akishalemewa na tembo yeye huwa kama kidau cha mpamba. 'Kidau cha mpamba' ni fumbo linaloashiria kuwa mlevi huwa anayumbayumba kama kidau chepesi kilichoundwa kwa pamba. Kidau hiki hupindukapinduka kikiwa majini. Huwa kinazidiwa na mawimbi ya majini. Siti anahusisha hali hii ya kidau cha mpamba na mlevi. Mfano katika ubeti:

*Ukuti wa mnazi ukiingia upepo
Unatetema, kidau cha mpamba
Usitukane wakunga na uzazi ungalipo*

Siti katika kauli 'kidau cha mpamba ukipakia mawe', anadhihirisha jinsi ambavyo walevi hujitesa kupitia pombe. Kidau cha mpamba kwa hali ya kawaida hakipo lakini ishara ya pamba ni kuashiria kitu chepesi ambacho hakiwezi stahimili uzito wowote. Kupakia mawe inaashiria kubugia ulevi. Siti anaona kileo ni kama jiwe ambalo linazidi dau uzito. Mlevi hana uwezo wa kujimudu akiwa amebugia tembo. Neno mwiko ni kifaa cha mti chembamba upande wa mshikio na bapa upande mwingine ambacho hutumikahasa kwa kusongea au kupakulia chakula. Kifaa hiki ni muhimu katika kufanyia shughuli za kupakulia na kukoregea chakula kikiwa chunguni au kwenye sufuria. Katika kauli hii ya Siti Binti Saad ya 'sijauramba mwiko', alimaanisha kuwa hajaonja pombe. Yeye alikuwa bado makini katika akili zake hana athari ya ulevi. Ingawa anaashiria kuwa muhogo wa Jang'ombe ni mtamu na mara nyingi wapishi wasipochunga hujikuta wameuramba mwikowakati wa kupakuwa. Hii ni ishara kuwa pombe ya kutoka Jang'ombe ni tamu na ina majaribio.

'Usitukane wakunga, uzazi ungalipo' ni methali katika mawasiliano ya kawaida. Lakini katika wimbo huu inajitokeza kama fumbo. Maana ya methali hii ni lazima ihusishwe na mafumbo mengine katika wimbo huu ndiyo maana yake iweze kufumbika. Hili ni fumbo la kimethali. Wakunga katika wimbo huu ni wapenzi wanawake na watoto ambao wanadharauliwa na wanaume wakisha kuwa walevi.

Tabia za mlevi baada ya kulewa zilijitokeza kupitia kwa kifungu 'kidau kinaenda hicho kinazama'. Fumbo hili linaashiria jinsi ambavyo mlevi hujipata baada ya kuzidiwa kwa tembo. Yeye huregea na kuanza kuwa na shida ya kutembea. Hutembea akiegemea upande mmoja na mwisho huanguka chini. Ulevi humfanya mtu kuwa mnyonge na kuisha nguvu za kujimudu wakati wa kutembea. Kuzama kwa kidau ni kuanguka kwa mlevi anapozidiwa na kileo.

Hali hii ya ulevi iliendelezwa na mshororo 'ukuti wa mnazi ukiingia upepo unamtetema'. Ukuti ni jani la mnazi likiingwa na upepo hupeperushwa. Katika wimbo huu Siti alikuwa akiashiria jinsi ambavyo mlevi huwa baada ya kubugia mvinyo. Yeye huishiwa kwa nguvu na huwa amelemewa zaidi. Ukuti wa mnazi ni fumbo ambalo linaashiria mtu mlevi ilhali upepo ni kileo ambacho mlevi anabugia. Fumbo hili lilifanya wimbo huu ukawa marufu sana mpaka sasa ubeti huu wa *ukuti wa mnazi* bado unaimbwa na watoto wakiigiza tabia ya walevi kuanguka (Nasra 2007: 61).

Wimbo 'Wewe Paka'

Wanawake ambao hawakuwa wameolewa kutoka kwa jamii zilizotengwa kwa msingi wa umasikini walipata wakati mgumu sana. Walijipata katika hali ya utongozwaji isiyofaa. Kwa mjibu wa Fair (2013: 52) wanaume walijenga dhana kuwa umaskini wa mwanamke haukumruhusu kusema 'hapana'. Siti naye hakusazwa katika hali hii. Nasra (2007: 78) anasema kuwa kuna mwanamume mmoja bwenyenye ambaye alitaka kufanya mapenzi na Siti lakini Siti akakataa. Mwanamume huyu alikasirika sana na akatangaza kuwa atalipia faini mtu yeyote atakaye mpiga Siti na ahukumiwe. Siti alitunga wimbo huu *Wewe Paka* kukashifu hali hiyo mbaya. Mwanamume huyu alitaka kutumia nguvu zake na kujaribu kumfunga Siti jela ilhali yeye ndiye mkosa. Naye Siti alilemewa kumfunga jela mshukiwa huyu bwenyenye lakini akamwachia mwenyezi Mungu. Hasimu huyu wa Siti alikaripiwa na jamii kwa tendo hili. Siti akawa huru mjini akirandaranda bila uoga wala wasiwasi.

Neno 'paka' katika muktadha wa wimbo huu limetumika kama fumbo. Paka kwa kawaida ni mnyama anayefugwa nyumbani. Paka humtegemea binadamu kwa mlo au abahatike katika mawindo yake kumpata panya kama kitoweo. Mfano katika ubeti:

Wewe paka kwani waniudhiyani

Wewe paka waudhi majirani

Utapiywa ukalipiwe faini

Ukalipiwe faini...

Mimi paka sasa napigiwani

Katika wimbo huu, Siti amejitambulisha kama 'paka' kwa vile amedharauliwa na mwanamume wa kibwenyenye kwa kutaka kumdhulumu kimapenzi. 'Paka' ni kitambulisho cha watu wenye tabaka la chini katika jamii. Siti alitambulisha wanawake maskini katika enzi hizo vile walivyodharauliwa. Nasra (2007:80) anasema kuwa kupitia wimbo huu wa *Paka*, Siti aliwatetea wanawake wengine ambao walipitia hali hii ya dhuluma ya kimapenzi. Siti anaendeleza malalamishi kwa ubeti ufuatao:

Mimi paka sasa napigiwani

Mimi paka sili cha mtu sinani

Nnajuta kuingiya vibandani

'Ninajuta kuingia vibandani', nikauli nyingine ambayo ina maana fiche. Kibanda kwa kawaida ni sehemu ambayo ni duni kwa maisha ya binadamu. Binadamu wa kiwango cha chini maishani

waliishi katika sehemu kama hizi. Mitaa duni huhusishwa na neno hili yani mitaa ya mabanda. Katika wimbo huu wa *Wewe paka* Siti anajuta kutoka kwa jamii maskini. Mama yake alikuwa akishughulika na biashara ya kuuza viungu na kipato chake kilikuwa cha chini sana. Siti ndoa yake ya kwanza ilivunjika kwa kukosa njia za kukimu familia yake. Kwa hivyo, neno kibanda ni kitambulisho cha umaskini katika wimbo huu.

Siti anasema kuwa yeye kama maskini au mtu dhaifu hana kosa lolote kustahili kupigwa. Yeye hajamkosea mtu yeyote. Kumkosea mtu ndiko kunahusishwa na kauli hii ya 'mimi paka sili cha mtu'. Mara nyingi mtu au mwizi hupigwa kwa kuiba vitu vya watu. Hata hivyo, Siti hana kosa lolote ila tu kwa kuwa yeye ni maskini ndilo kosa lake. Katika wimbo huu Siti anazungumzia kuhusu mapenzi yake kutoka kwa bwanawake. Anasema kuwa mapenzi yake hayapo tena. Ni huzuni kwake kutopata mpenzi anayeweza kumuauuni. Mambo hayamuendei Siti vizuri. Penzi ambalo lingempa furaha limeharibika kwa hivyo anahusisha penzi kuharibika na tiba iliyo na huzuni. Mfano katika ubeti:

Langu tiba imeingiwa huzuni

Matilaba nimeyapata zamani

Ukizinga utarejea ngamani

Utarejea ngamani

Siti alitumia msitari 'ukizinga utarejea ngamani' kumaanisha kuwa dhuluma wanayopata kama akina mama wa tabaka la chini itaendelea kuwepo wasipoipinga. Fumbo hili lina maneno mawili muhimu ya kueleza. Kuzinga ni kitendo cha kuzuia kuona mbele ilhali neno ngamani ni sehemu ya katikati ya meli. Kwa hivyo, Siti aliiashiria kuwa iwapo hangeungwa mkono na akina mama kwasuala la dhuluma ya kimapenzi kutoka kwa mabwenyenye wangerejea palepale.

Wimbo Suhuba ya Dai

Siti Binti Saad anazungumza kuhusu mwanamke ambaye yumo katika ndoa iliyo na utata. Anapata hali ngumu kutoka kwa mumewe ambaye anamtusi. Hali hii ya matusi ni ngumu na ilimshinda kuvumilia. Aliamua kumkimbilia rafiki yake ambaye aliamini angemfaa kwa halina mali kwani undugu si kufanana ila ni kufaana. Au rafiki ni yule akufaaye kwa dhiki. Kwake anaona kuwa urafiki ni ule wa kutendana mema na kufaana. Hali hii ya urafiki inampelekakwa rafiki yake ili amkomboe katika lindi la shaka ya ndoa. Anasema kuwa wakati mwingine penzi huweza hata kuua bila kutarajiwa. Anamkumbusha rafiki yake kuwa hali au tabia za bwanake si nzuri na ni ishara ya jambo baya katika ndoa. Anaona ni vyema rafikiye amshauri ili aweze kumuokoa katika hali hii.

Anaendelea kudai kuwa amevumilia kwa muda hali hii ya matusi ya bwanake lakini ameshindwa kwani tabia hizi bado zipo na haziishi. Amekuwa akivumilia katika ndoa ili kuweza kutulia na kufurahia ndoa yake lakini tabia za matusi bado zipo. Hali hii inakuwa ngumu kwake na inampelekea kuomba msaada. Anafurahi kuwa na rafiki wa dhati na anaamini amamfa. Anamwomba rafiki huyu aende amwambie bwanake ukweli kuwa tabia ya kutomsaidia katika ndoa licha ya kuishi pamoja kama waandani si nzuri.

Anwani ya wimbo huu 'suhuba ya dai' imejitokeza kama fumbo, kwa vile maana yake haiko wazi wazi. Maana yake imefichwa kwa vile ni lazima mtu ajiulize ni suhuba ipi ya dai. Suhuba ni neno la Kiswahili lenye maana ya urafiki, sahibu, somo au mwandani. Dai pia ni neno la Kiswahili lenye kumaanisha kuhitaji kulipwa au kupewa haki fulani. Kwa hivyo, katika wimbo huu urafiki ni kama kuwa na deni na mtu. Urafiki ni ule wa kusaidiana kwa maana ya ndani. Kwa hivyo, dai la

urafiki ni kusaidia. Katika wimbo huu mwimbaji anataka rafiki yake ampokee kwa usaidizi kwa vile bwanake hamthamini tena. Anaishi kwa mateso ya kutusiwa katika ndoa. Dai lake kwa rafiki yake ni kumuauni katika penzi ambalo linaweza kumuua.

Neno 'ninakuangukia' limejitokeza kama fumbo katika wimbo huu. Kuanguka ni kitenzi chenye maana ya kukosa kufaulu au kuteleza kisha ujipate uko chini. Kitenzi kimetumika katika wakati uliopo. Kumaanisha hicho kimetendeka lakini akajipata amemwangukia mwenzake kama kizuizi asiumiye. Mfano katika ubeti:

*Nawe zingatia yote hayafai
Ninakuangukia ninakuangukia ninakuangukia
Mno nafurahi mno nafurahi*

Katika wimbo huu mwimbaji anapokosana na bwanake kwa mateso ya matusi na kutosaidiwa katika maisha ya ndoa, anaona afadhali apate penzi kwingine kushinda kumpa bwanawake. Alimpigia magoti mwenzake kwa kuomba msaada wa kunasua familia yake. Anataka rafiki yake aende amwambiye bwanawake mambo haya bila uoga. Kwa kufanya hivi atakuwa amemwauni katika penzi ambalo linaweza muuwa. Siti katika wimbo huu alitumia kauli 'kupata kupoa' kuashiria furaha katika ndoa. Kupoa ni kumaanisha kuwa kitu chenye moto kinapopungukiwa na moto basi huwa kimepoa. Kile kisichokuwa moto huwa kimepoa. Katika wimbo huu mwimbaji anaelewa hali ya bwanake ya usumbufu na ameishi naye akidhani tabia hiyo itaisha lakini bado ipo. Alifanya hivi ili kuweza kufurahisha nafsi yake. Kufurahisha nafsi yake au kutulia ni kupata kupoa. Tazama ubeti huu:

*Nipate kupoa, nipate kupoa,
Nipate kupoa, nipate kupoa
Juu ya kukubali, juu ya kukubali
Nipate kupoa, nipate kupoa*

Katika wimbo huu *Suhuba ya Dai* kitenzi 'ashairejea' kimetumika mara kadha kama kiwakishi cha tabia fulani. Hiki ni kitenzi cha Kiswahili chenye kumaanisha kutenda kitu mara ya pili au zaidi. Katika wimbo huu limetumika kama fumbo kwa vile mwimbaji hasemi kipi kinarejeshwa wazi wazi. Lakini kile anachozungumzia ni tabia ya matusi ya bwanake katika ndoa.

Wimbo 'Kikombe cha zari'

Wimbo huu ni mojawapo wa nyimbo za Siti uliozungumzia kuhusu sifa za mwanamke kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja. Katika wimbo huu, Siti anajadili jinsi ambavyo wanawake hutumia urembo wao kuweza kujinufaisha kimapenzi. Kinyume na mtazamo kuwa, kitambo wanawake hawakuwa na uwezo wa kujiamulia kuhusu mpenzi. Wimbo huu unaashiria kuwa wanawake walikuwa na uhuru wa kuzunguka wanaume na kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja. Hali ya ugumu wa kiuchumi ndiyo iliyopelekea wanawake wengi kujiingiza katika tabia hii ya kuwa na wanaume wengi. Wimbo huu ulihusisha tabia ya wanawake kutoka mashambani na Ngambo ambapo hali ya kiuchumi ilikuwa duni. Kwa mjibu wa Fair (2013) wimbo huu uliimbwa ili kudhihirisha hali halisi ya kisiasa na kijinsia ya wakati huo. Wanawake baada ya kuondolewa kwa biashara ya utumwa nao walitaka kujikomboa kimaisha na kiuchumi. Walitumia wanaume kama kitega uchumi wao. Nyimbo hizi zinaonyesha kuwa wanaume waliumia katika harakati za mapenzi hasa walipoachwa na wapenzi.

Anwani ya wimbo huu *Kikombe cha Zari* ina maana fiche. Kikombe cha zari ni aina ya kikombe kidogo cha chai kilichonakishiwa nakshi maalum kwa rangi inayofanana na rangi ya dhahabu. Vikombe hivi huvutia sana. Viliikuwa ni aina ya vikombe maarufu na vilipendwa kutumika katika jamii ya Unguja. Bado kwa sasa vinatumika ingawa hadhi yake si kama ilivyokuwa mwanzo. Kikombe cha zari cha chai hupendeza na hata humfanya mnywaji chai kuwa na hamu nyingi ya kunywa chai. Kikombe hiki wakati mwingine hupakwa kwa madoadoa ya jaribosi. Kikombe hiki kinaashiria mwanamke mrembo ambaye anatamaniwa na mwanamume kwa mapenzi. Kwa kawaida kikombe huwa ni cha kunywa maji au chai. Kwa hivyo, kile ambacho kinahifadhiwa pale ni cha thamani kwa mnywaji. Siti alitambulisha mwanamke mrembo kama kikombe cha zari. Tazama ubeti ufuatao:

Kikombe cha zari

Kizuri kwa chai

Utie maziwa

Na nyingi sukari

Ukiondoka wewe

Mwengine tayari

‘Chai’ inaashiria mapenzi ambayo yanapatikana kwa mwanamke mrembo. Mahaba matamu ambayo yanatokana na urembo wa mke au mpenzi. Chai hunywewa na watu ikasaidia kupoza njaa vile mapenzi hupoesha mtu mwenye kiu cha mapenzi. Mapenzi ambayo mtu hupata kwa mpenziwe ndiyo Siti anarejelea kama chai. Siti anapendekeza kuwa iwapo unataka chai iwe tamu, ni lazima ‘utie maziwa na nyingi sukari’. Chai iliyoandaliwa kwa maziwa na sukari nyingi huwa tamu sana. Mwanamke anataka mume wake alete viambata hivi kwa maandalizi ya chai tamu. Maziwa na sukari ni vitu ambavyo wanawake walitaka kufaidi kutokana na mapenzi yao kwa waume. Kulingana na Siti, ili mapenzi yawe matamu ni lazima mwanamume ajikaze kwa kutoa pesa au vitu vya thamani kwa mwanamke. Wanawake walitaka kujijenga kifedha kupitia mapenzi. Mfano katika ubeti:

Kikombe cha zari

Kizuri kwa chai

Utie maziwa

Na nyingi sukari

Ukiondoka wewe

Mwengine tayari

Wimbo ‘Kigalawa’

Wimbo huu ulitungwa kuashiria kuwa, masikini na tajiri walihitaji kutangamana bila matatizo yoyote. Binadamu wote wanahitaji hadhi na heshima. Siti na kikundi chake waliimba wimbo huu walipoalikwa kumtumbuiza Sultan Seyyid Khalifa na mke wake Bibi Matuka katika kasri lao (Fair 2013). Siti anasema kuwa atatumia kigalawa kuvuka ng’ambo nyingine kumueleza mfalme masaibu yao ya kuwa watumwa. Amebeba mzungo mdogo ambao angeutumia kulipia kama poni. Anakubali kulipia nusu pauni ili kujiepusha na shida ya utumwa. Anasema kuwa yeye atatumia vizuri rasilimali ambazo yuko nazo na anasema hakopeshi wala hauzi mali yake. Anaendelea kusema kuwa kazi yake ni kuliwaza wale ambao wanalalama au kulia. Aliwahimiza wenzake wachochole watafute shughuli muhimu ya kufanya ili wajitegemee waache kulalamika. Mafumbo katika wimbo wa Kigalawa:

Kigalawa ni chombo cha usafiri majini, Siti anajilinganisha na kigalawa. ‘Kigalawa’ kinaashiria

watu wa tabaka la chini. Siti anaona kuwa kigalawa ni kidogo lakini pia kiruhusiwe kusafiri baharini katika shughuli ya kuchuma mali. Hali ya wakaazi wa Ng'ambo ambako Siti alitoka ilikuwa ngumu sana na utabaka ulikuwa umewakandamiza zaidi. Siti alikuwa akipigania haki ya watu wa tabaka la chini ili wawe huru wakichuma mali yao. Mfano katika ubeti:

Kigalawa sawa sawa na chombo

*Baharini huenda mirengo mirengo
Sivuwani shuka ya sitiri mambo*

Siti anahusisha uwezo wa kigalawa na vyombo vingine vya majini. Anaona kuwa hata maskini au watu wanyonge wana uwezo wa kuchuma mali. Kuwa na 'vitu ndani kwa kigalawa' kunaashiria kuchuma mali. Mali hii inaweza kutumika kulipia poni. Siti anaashiria kuwa kigalawa kama vyombo vingine vya majini kina hadhi na thamani yake. Masikini pia wanahitaji kupewa heshima kwani wana thamani yao katika dunia. Tazama ubeti ufuatao:

Kigalawa kumbe kina vitu ndani

*Unitweke hata kwa mwinye Husseni
Japo moto sinitia kisimani
Kigalawa ulete mali kapuni
Ni tajiri takupa nusu pauni
Yangu ya mkufu upate kuweka poni.*

Maisha yao na watu matajiri ni sawa. Shida ambazo matajiri wanapitia maishani ndizo masikini wanakumbana nazo. Hali hii ya matatizo ya tabaka hizi mbili Siti alifumba kwa kusema, 'baharini huenda mirerengo'. Mfano katika ubeti:

*Kigalawa sawa sawa na chombo
Baharini huenda mirengo mirengo
Sivuwani shuka ya sitiri mambo*

Siti anasema kuwa ni vyema kuwe na ushirikiano kati ya tajiri na maskini. Hali hii ikitokea jamii itanawiri vizuri. Siti anajenga ujumbe huu kwa kusema 'moto sinitia kisimani'. Moto unatarajiwa kuangaza vizuri kisimani ili shughuli ziendeleo lakini iwapo hakuna maelewano basi moto utazimwa na maji ya kisima. Moto ukizimwa basi shughuli zitagonga mwamba kwa kukosekana mwangaza.

Wimbo Umuongo Basahera1

Bwana mmoja anatamani kupata mke lakini hajui jinsi ya kumnasa. Shida yake ni kuwa anajifanya kuwa anajua kumbe hajui. Siti anataka kumuonyesha jinsi ya kumnasa mke mzuri. Anamshauri kuwa si njia moja pekee inaweza kumwezesha kupata mke. Bwana huyu anaambiwa kutafuta maarifa mengi na baadaye ataweza kupata mke. Pia Siti anamueleza kuepuka kutafuta wake ambao si wa kufu yake. Ujuzi wa kupata mke ni ujishughulishwa kwa kutumia vishawishi vizuri ili viwapendeze wanawake. Vishawishi hivi ni kama maneno mazuri. Mafumbo katika wimbo huu:

Nyumba katika hali ya kawaida haiwezi jengwa na kijiti kimoja. Ni sawa na meko, hayawezi injikwa na jiwe moja. Kijiti kimehusishwa na njia ya kumshawishi mke. Siti anaposema kuwa 'kuna kijiti kimoja kitasawisha jengo?' Anamaanisha kuwa njia moja haiwezi kutumika kumpata mke. Njia

nyingi zinahitajika. Jengo katika muktadha huu linamaanisha ndoa au muungano wa maelewano ya mapenzi kati ya mke na mume. Mume anahitajika maarifa mengi ili kuweza kumrai mke ampendaye. Mfano katika beti:

Umuongo basahera umuongo
Kuna kijiti kimoja kitasawisha jengo
Huna pau huna mzigu huna nyongo
Nenda ukakate miti nije nikuone jingo

Mwanamume anahimizwa kutafuta ujuzi mwingi wa kuweza kumnasa mke. Siti anawasilisha suala hili kwa kusema ‘nenda ukakate miti nije nikuone jengo’. Miti kwa hali ya kawaida hutumika katika ujenzi. Katika muktadha wa wimbo huu hali ya kukata miti imehusishwa na maarifa ya kupata mke. Bwana huyu akipata maarifa mengi bila shaka atawezewa kupata jiko lake. Kujenga jengo kuna maana ya kupata jiko. Mfano katika ubeti:

Umuongo basahera umuongo
Kuna kijiti kimoja kitasawisha jengo
Huna pau huna mzigu huna nyongo
Nenda ukakate miti nije nikuone jingo

Mwimbaji anamwonya bwana huyu asipate mke ambaye si wa kiwango chake, anasema ‘paka nakukanya usirambe tui’. Tui hutokana na kukunwa kwa nazi. Hutumika katika mapishi, ni kiungo kimojawapo muhimu cha mapishi. Tui si chakula cha paka. Paka mara nyingi amezoea maziwa wala si tui. Tui inahusishwa na maana ya mwanamke ambaye si kufu au kiwango cha bwana huyu ambaye hajui kuwarai wake. Tui ni mwanamke ambaye si wa kiwango cha bwana huyu anaweza kuwa amemzidi kwa ujanja au hali ya maisha. Mfano katika ubeti:

Paka nakukanya usirambe tui
Ukajinyongonya mengi huyajuwi
Kama huli panya na wali huperi jamani
Umuongo basahera umuongo

Tabia ya bwana huyu kuepuka wake wa kiwango chake na kuendea wale wanaomzidi, mwimbaji ameifumba kwa kusema ‘huli panya na wali huperi’. Chakula cha paka ni panya. Paka amehusishwa na bwana huyu ambaye hajui kuwashawishi wake. Chakula chake cha kawaida huwa ni panya. Panya anahusishwa na wake ambao ni wa kufu wa huyu bwana. Bwana huyu anatafuta wali, chakula ambacho hapendi. Wali ni mke ambaye si kufu ya bwana huyu. Siti anapendekeza kwa bwana huyu njia ya kupata mke. Anamshauri kuwa ‘kutagua togoo Chambo kiwe kingi’. Chambo kwa mujibu wa Nabhany (2012) ni aina ya chakula cha kuwatilia samaki katika ndowana kwa ajili ya kumkamata. Kuna Chambo cha dome, kamba, ngisi na pweza wakati wa kuvua. Chambo kina husishwa na njia nyingi za kutumia kumnasa mke. Siti anahimizwa bwana huyu kuwa na njia nyingi za kumnasa mke. Mfano katika ubeti:

Tagua togoo chambo kiwe kingi
Upate chatoo na kamba wa lulu
Jamani jongoo hatiwi mtungi

Mwimbaji anapendekezea bwana huyu awatafute wanawake wa kufu yake, kwa kumwambia kuwa 'upate chatoo na kamba wa lulu'. Chato na kamba ni aina ya samaki ambao watu hufurahia kitoweo chao. Samaki hawa wanalinganishwa na mwanamke mzuri wa kitabia na kufu wa bwana huyu. Kamba wa lulu ni mwanamke mwenye haiba nzuri lakini ni wa kiwango cha bwana huyu.

Hitimisho

Makala hii imeshughulikia mafumbo katika nyimbo za Siti Binti Saad. Maana katika mafumbo haya yameelezwa kwa utaratibu wa wimbo baada ya wimbo. Maana ya mafumbo haya yamehusishwa na matokeo katika jamii na mandhari ya jamii husika. Kwa hivyo, ilidhihirika kuwa ili kuelewa mafumbo vizuri ni vyema mtu kufahamu utamaduni wa msanii vyema. Utamaduni alimokulia Siti ulikuwa wa maana katika kufahamu mafumbo katika nyimbo zake.

Marejeleo

- Bakhtin, M. (1981). *Theory of the Text*. Routledge.
- Bathes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. University of California Press.
- Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style*. Hatier Publications.
- Enon, J. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Makerere University.
- Fair, L. (2013). *Historia ya Zanzibar na Nyimbo za Siti Binti Saad*. Twaweza Publishers.
- Fromkin, V. Rodman, R. & Hymes M. (2003). *An Introduction to Language*. Thomson/Heinie.
- Githonga, W. N. (2013). *Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Issa, M. (1991). *Jukwaa la Taarab Zanzibar*. Mediafrica.
- I- Wensu, L. (2002) *What can Metaphor Tell us About culture?* National Tainwan University Language and Linguistics, 3(3), 589-612.
- Jilala, H. (2008). *The Artist Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (Haijachapishwa).
- Kahigi, K. K. na Mulokozi, M. M. (1982). *Kunga za Ushairi na Diwani ya Yetu*. Tanzania Publishing House.
- Kaneko, M. (2012). *Metaphor and Symbol*. University of the Witwatersrand.
- Kea, P. (2006). *Usemezano katika Nyimbo za Taraab*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- King'ei, K. (1993). *Language, Culture and Communication: The role of Swahili Taarab Songs in Kenya 1963-1990*. Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Howard.
- Kipacha, A. (2015). *Taswira za Ndege katika Maandiko ya Shaaban Robert*. Swahili Forum. 22, 1-19.
- Khamis, W. A. (2016). *Kuchunguza Dhamira za nyimbo za Siti Binti Saad*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Tanzania. (Haijachapishwa).
- Khamis, S. A. M (2004). *Versality of Taarab in Relation to Local and Global Influences*. Swahili Forum 11. P. 3-37.
- Khatib, M. (1992). *Taarab Zanzibar*. Tanzania Publishing house.
- Kothari, R. (2004). *Research Methodoly: Methods and Techniques*. New Age International Ltd.
- Lakoff, G. & Jonson M. (1980). *Metaphors we live by*. University of Chicago Press.
- Leech, G (2008). *Language in Literature*. Pearson Education Limited.
- _____ (1969). *A linguistic Guide to English Poetry*. London. Longman.
- Leech, G. & Short, M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose*. Longman Limited.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. East Africa Education Publishers.
- Nasra, H. M. (2007). *Mfinyazi Aingia Kasri: Siti Binti Saad, Malkia wa Taarab*. Mkuki na Nyota Publishers.
- Nguti, M. (2013). *Ulinganishaji wa Matumizi ya Tasfida za Mukdadha wa Nyumbani katika Lugha ya Kikamba na Kiswahili*. Tasnifu ya M. A (Haijachapishwa).
- Ntarangwi, M. (2001). *A socio-historical and contextual Analysis of Popular Musical Performance Among the Swahili of Mombasa*. Kenya, Cultural Analysis, 2, 1-37.
- Roberts, S. (1967). *Diwani ya 3: Wasifu wa Sinti Binti Saad*. Printpak Tanzania Limited.
- Roberts, S. (1991). *Wasifu wa Sinti Binti Saad*. Mkuki wa Nyuki.
- Shaban, M. (1966). *Waimbaji wa Juzi*. Chuo Cha Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.
- Sheikh, S. (1994). *Yanayoudhi Kuyaona Mafumbo na Vijembe vya Kiswahili AAP (7-11) Swahili-Kolloquium*.
- Timammy, R. (2002). *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A stylistic Analysis*. Tasnifu ya Uzamifu

Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

Vierke, C. (2012). *Mafumbo: Considering the Functions of Metaphorical Speech in Swahili Contexts*. Annual Conference on African Linguistics, 42, 278-290.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix.

Wardhaugh, R. (2002). *An Introduction to Sociolinguistics*. (4th Ed). Oxford: Blackwell Publishers.